

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 45 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) NOVEMBA 2024

TSC YAADHIMISHA SIKU YA WALIMU DUNIANI KWA KUENDESHA KLINIKI YA KUTOA HUDUMA KWA WALIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akimwonesha nyaraka mbalimbali zinazohusu utumishi wa walimu zilizopo kwenye tovuti ya Tume Mwalimu Kefa Kitutu aliyetembelea Kliniki ya kutoa huduma kwa walimu iliyoendeshwa na TSC kuanzia tarehe 5 hadi 11 Oktoba, 2024 katika ofisi za Tume hiyo jijini Dodoma.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

KONGOLE TSC KWA KUTOA MAFUNZO KWA WAKUU WA SHULE

Hivi karibuni Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo Wakuu wa Shule za Msingi kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na ufanisi katika kusimamia walimu wanaowaongoza.

Mafunzo hayo yana lengo la kumwezesha kila Mkuu wa Shule kusimamia masuala mbalimbali yanayohusu maadili na nidhamu kwa walimu.

Mafunzo hayo ni nyenzo muhimu ya kuwezesha Wakuu wa Shule kuhakikisha walimu wanatekeleza wajibu wao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo, na hivyo itasaidia kupunguza

mashauri ya nidhamu kwa walimu.

Pamoja na hayo, mafunzo hayo yamesaidia Wakuu wa shule kujiamini pale inapohitajika kumchukulia hatua za kinidhamu mwalimu kwa kwenda kinyume na maadili ya kazi.

Tunatoa pongezi kwa Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuona umuhimu wa kutoa elimu kwa viongozi hao wa shule. Matarajio yetu ni kuona Wakuu wa Shule wanajenga mazingira rafiki kwa walimu wanaowaongoza ili kila mwalimu atekeleze majukumu yake kwa furaha na amani na kuondokana na changamoto za utovu wa nidhamu kwa baadhi yao.

KATUNI



Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



TSC YAADHIMISHA SIKU YA WALIMU DUNIANI KWA KUENDESHA KLINIKI YA KUTOA HUDUMA KWA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Katika kuadhimisha Siku ya Walimu Duniani, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliendesha Kliniki ya kutoa huduma kwa walimu na wadau mbalimbali iliyofanyika kwa siku saba kuanzia tarehe 5 hadi 11 Oktoba, 2024 katika Ofisi za TSC Makao Makuu jijini Dodoma.

Akizungumza na vyombo vya habari tarehe 5 Oktoba, 2024, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema walimu wanakaribishwa kufika katika kliniki hiyo kupata elimu na kutatuliwa changamoto za kiutumishi zinazowakabili.

Alisema TSC ni mdau muhimu katika kuadhimisha Siku ya Mwalimu Duniani kwa kuwa kwa walimu walioajiriwa katika utumishi wa umma wanaofundisha kwenye shule za Msingi na Sekondari Tanzania Bara wanahudumiwa na Tume ya Utumishi wa Walimu ambapo kwa sasa Tume inahudumia walimu 274,541 huku walimu 180,325 wakiwa ni wa shule za Msingi na 94,216 ni wa shule za Sekondari.

Akizungumzia namna Serikali kupitia TSC inavyoshughulikia maslahi ya walimu, Mwl. Nkwama alisema Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan jumla ya walimu 37,473 wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

“Kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 walimu waliopandishwa vyeo ni 126,346, mwaka 2021/2022 walimu waliopandishwa vyeo ni 35,112, mwaka 2022/2023 ni 65,925 na mwaka 2023/2024 walipandishwa vyeo walimu 158,916. Aidha, katika kipindi hicho walimu 25,006 wamebadilishiwa vyeo baada ya kujiendeleza kielimu,” alisema.

Aliongeza kuwa Tume hiyo imefanya ziara shuleni kwa ajili ya kutoa elimu na Ufafanuzi wa Kanuni



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akitoa ufafanuzi kwa mteja, Mwl. Kefa Katutu (kulia) aliyetembelea Kliniki ya kutoa huduma kwa walimu iliyoendeshwa na TSC kuanzia tarehe 5 hadi 11 Oktoba, 2024 katika ofisi za Tume hiyo jijini Dodoma. Pichani, kushoto ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Chamwino, Mwl. Paulina Kanumba.

za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu ili kuwawezesha kuelewa wajibu na haki zao kwa lengo la kuwaepusha walimu kufanya makosa yanayosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu, ambapo jumla ya walimu 265,880 wa shule za msingi na sekondari walifikiwa.

Kwa mujibu wa Mwl. Nkwama, TSC imefanikiwa kujenga Mfumo wa kielektroniki wa TSCMIS-Teachers Service Commission Management Information System wenye lengo la kuboresha utendaji kazi katika kuwadumia walimu kwenye masuala ya Ajira na Maadili.

“Serikali kupitia Mradi wa BOOST imeipatia Tume jumla ya magari 11 kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma kwa walimu ngazi ya wilaya na Makao Makuu, kuwajengea uwezo jumla ya wajumbe 426 wa Kamati za Tume za Wilaya za Ajira, Upandishwaji vyeo na Nidhamu ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia utumishi wa walimu,” alisema Katibu huyo.

Aidha, Mwl. Nkwama alisema, TSC inatarajia kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wakuu wa shule 3,066 ili kuwawezesha kusimamia masuala ya Maadili kwenye ngazi za

shule kwa kuzingatia kuwa wao ni Mamlaka ya Nidhamu ngazi ya shule. Aidha, Tume imeandaa na kusambaza jumla ya vitabu 20,000 kwenye shule za Msingi Tanzania Bara kuhusu ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu.

“Vilevile Tume kupitia Mradi wa SHULEBORA imefanikiwa kuandaa na kuchapisha vitabu 200 kuhusu ufafanuzi wa masuala muhimu yaliyomo katika Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016. Tume pia kwa kushirikiana na World Vision imefanikiwa kuandaa kitini cha kufundishia walimu wa shule za Msingi na Sekondari masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya walimu,” alisema.

Siku ya Walimu Duniani huadhimishwa tarehe 5 Oktoba ya kila mwaka ikiwa ni kumbukumbu ya kupitishwa kwa Pendekezo la ILO/ UNESCO mwaka 1966 kuhusu Hadhi ya Walimu lililoweka viwango vya Haki na Wajibu wa Walimu.

Pendekezo hilo huangazia viwango vya mafunzo ya Taaluma ya ualimu, Mafunzo kazini, Ajira pamoja na Masharti ya Kufundishia na Kujifunzia huku likitambua mchango wa Walimu katika kuboresha Elimu na kujadili maslahi yao.



Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Ajira na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Mectildis Kapinga (kulia) akifurahia jambo na mteja aliyetembelea Kliniki ya kutoa huduma kwa walimu iliyoendeshwa na TSC kuanzia tarehe 5 hadi 11 Oktoba, 2024 katika ofisi za Tume hiyo jijini Dodoma.



Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Maadili ya Walimu wa TSC, Mwl. Asha Lubuva (kulia) akimsikiliza mteja aliyetembelea Kliniki ya kutoa huduma kwa walimu iliyoendeshwa na TSC kuanzia tarehe 5 hadi 11 Oktoba, 2024 katika ofisi za Tume hiyo jijini Dodoma.

Afisa Utumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bibi Elieth Ntinabo (kulia) akimhudumia mteja aliyetembelea Kliniki ya kutoa huduma kwa walimu iliyoendeshwa na TSC kuanzia tarehe 5 hadi 11 Oktoba, 2024 katika ofisi za Tume hiyo jijini Dodoma.



Afisa Utumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bibi Dunia Nampanga (wa kwanza kulia) akifafanua jambo kwa mteja aliyetembelea Kliniki ya kutoa huduma kwa walimu iliyoendeshwa na TSC kuanzia tarehe 5 hadi 11 Oktoba, 2024 katika ofisi za Tume hiyo jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia) akiwa pamoja na watumishi wengine wa TSC tayari kwa kutoa huduma kwa wateja wanaotembelea Kliniki ya kutoa huduma kwa walimu iliyoendeshwa na TSC kuanzia tarehe 5 hadi 11 Oktoba, 2024 katika ofisi za Tume hiyo jijini Dodoma.

WALIMU NCHINI WAUNGANA NA WENZAO DUNIANI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MWALIMU



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza kwenye Maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani ya mwaka 2024, yaliyofanyika katika mji mdogo wa Ushirombo, Wilayani Bukombe mkoani Geita, hivi karibuni. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

Na Mwandishi Wetu – Bukombe.

Siku ya Mwalimu Duniani huwa inaadhimishwa tarehe 5 Oktoba, ya kila mwaka ikiwa ni kutekeleza Azimio la UNESCO/ILO la mwaka 1966 kuhusu hadhi, haki na wajibu wa Mwalimu.

Walimu nchini waliungana na wenzao kushiri maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani ambayo kitaifa yalifanyika kwenye uwanja wa mpira wa shule ya sekondari Ushirombo, wilayani Bukombe, mkoani Geita huku ikiwa na kauli mbiu 'Mwalimu ni Nyota inayoangaza'.

Katika maadhimisho hayo, Mgeni Rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kasimu Majaliwa Majaliwa.

Akizunguza hivi karibuni wakati wa maadhimisho hayo, Mhe. Kassim Majaliwa alisema Serikali haijatoa maagizo ya kuwaondoa

kazini walimu wa cheti bali amewataka watumie mpango wa mafunzo endelevu kazini kwenda vyaoni kusoma.

"Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Mpango wanatambua mchango wa Walimu na wanathamini kazi zao. Serikali ya awamu ya sita itaendelea kuboresha maslahi ya walimu ili wafanye kazi kwa ufanisi," alisema.

Alisema Serikali imefanya maboresho ya sera na mitaala ya elimu nchini ambayo pamoja na mambo mengine imeleta mabadiliko katika sifa za chini za mwalimu katika shule za msingi kuwa Stashahada/Diploma. "Pamoja na mabadiliko haya, Serikali inatambua kuwa bado wapo walimu ambao hawajafikia sifa ya kuwa na Astashahada au Diploma na hakuna agizo la kuwataka waondolewe katika ajira," alisema.

Alisema walimu wote ambao

hawana sifa ya Astashahada au Diploma watumie fursa ya mpango wa mafunzo endelevu kazini kwenda vyaoni kusoma ili kupata sifa ya diploma au kujiendeleza kupitia moduli kwa mfumo wa LMs – Learning Management System chini ya Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE).

"Kupitia mfumo huu, Serikali imeingia makubaliano na kampuni ya simu ya Airtel kwa walimu wenye vishikwambi na wanatumia mtandao wa Airtel kupakua moduli bure kwa ajili ya kujiendeleza.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ameagiza TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, taasisi za elimu, sekta binafsi na wadau wa sekta ya elimu nchini wahakikishe walimu wanajengewa mazingira bora ya kazi ili watimize majukumu yao kwa ufanisi.

Aidha, aliwataka waimarishe programu za mafunzo kwa walimu ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia huku akiwataka waajiri kuwapa

WALIMU NCHINI WAUNGANA NA WENZAO DUNIANI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MWALIMU

mafunzo walimu pamoja na taasisi zinazohusika na udhibiti wa ubora waendeleo kutimiza majukumu yao.

Katika kuboresha sekta ya elimu nchini, Waziri Mkuu alisema Serikali imeendelea kuboresha na kusimamia miundo ya watumishi wakiwemo walimu. "Serikali imeboresha stahiki za msingi za watumishi kwa kupandisha madaraja na kuhakikisha wanapata nyongeza ya mishahara yao kwa wakati."

Aliongeza kuwa, "Serikali imeimarisha miundombinu mahali pa kufanyia kazi ikiwemo kuhakikisha kuna madarasa, maabara, mabweni, majengo ya utawala na sasa tumeingia kwenye ujenzi wa nyumba za walimu pamoja na kuimarisha ajira zao."

Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari kupitia miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP), Mradi wa Kuimarisha na Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (BOOST), Mradi wa Huduma za Maji, Elimu ya Afya na Usaifu wa

Mazingira (SWASH), Programu ya Uboreshaji Kada ya Ualimu (GPE – TSP) na Programu ya Kutekeleza Elimu kwa Matokeo (EP4R).

Akielezea kuhusu upandishaji madaraja kwa walimu, alisema: "Kati ya Machi, 2021 na Agosti, 2024, walimu 601,698 nchi nzima wamepandishwa madaraja na Serikali imetumia shilingi trilion 1.3 kuwalipa. Na niwatake Maafisa Elimu kuwatembelea walimu vijijini na kusikiliza kero zao," amesisitiza Waziri Mkuu.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Machi, 2021 hadi sasa, Serikali imeweza kuwabadilisha kada/miundo jumla ya watumishi 36,768 kwa gharama ya sh. 3,090,476,931.00 na imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 144,356 yenye jumla ya sh. milioni 229.9.

Akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na hadhara hiyo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko aliwashukuru walimu wa Tanzania kwa kuendelea kuiheshimisha taaluma yao na kuwa chanzo cha maarifa kwao hakitoki kwingine isipokuwa kwao hivyo wailinde

kwa wivu mkubwa taaluma hiyo.

Dkt. Biteko alisema mwaka 2015 wakati anachaguliwa kuwa Mbunge, wilaya yake ilikuwa ikishika nafasi ya mwisho katika mitihani ya Taifa. "Nilizungumza na walimu kuhusu matokeo mabaya na wakasema tusiwaache walimu nyuma hivyo tulianza kukutana na kufanya tathimini na sasa tunafanya vizuri."

Alisema viwango vya ufaulu vimekuwa vikiongezeka kila mwaka huku akitolea mfano wa matokeo ya mwaka jana kwamba darasa la saba wilaya hiyo ilishika nafasi ya pili katika mkoa huo, darasa la nne ilipata wastani wa asilimia 78 na kuwa nafasi ya pili kimkoa.

"Kidato cha pili tulikuwa na ufaulu wa asilimia 98, kidato cha nne ufaulu ulikuwa asilimia 96, kidato cha sita ulikuwa asilimia 100 na hizi zote tulikuwa wa kwanza. Katika mitihani ya mock ya kanda ambayo ilijumuisha mikoa mitano yenye Halmashauri 37, Wilaya ya Bukombe tumeshika nafasi ya tatu, tukiwa nyuma ya Ilemela na Nyamagana. Hivyo, niliona tutenge siku moja ya kusema asante mwalimu."

Aidha, Dkt. Biteko alisema kuwa walimu nchini wasivunjike mioyo waendeleo kufanya kazi yao na kuwa maisha yao ni kielelezo cha mafanikio katika Taifa na kuwa wao ni nyota inayoangaza na yeye ataendelea kushirikiana nao.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kama msimamizi wa walimu katika masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya walimu iliwakilishwa na Katibu wake, Mwl. Paulina Mbena Nkwama, Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Iddi Muya pamoja na Kaimu Katibu Wasaidizi wa Wilaya za Bukombe, Mbogwe, Geita, Chato na Nyang'wale.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akijadiliana jambo na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwenye Maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani kwa mwaka 2024, yaliyofanyika katika mji mdogo wa Ushirombo, Wilayani Bukombe mkoani Geita, hivi karibuni. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

WALIMU NCHINI WAUNGANA NA WENZAO DUNIANI
KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MWALIMU

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko akitoa maelezo mafupi kabla ya kumkaribisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwa ajili ya kuwahutubia Walimu wakati Maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani kwa mwaka 2024, yaliyofanyika katika mji mdogo wa Ushirombo, Wilayani Bukombe mkoani Geita, hivi karibuni. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akifafanuliwa jambo na Meneja wa Tawi la CRDB Bukombe, Lusajo Mwaijande, wakati alipotembelea mabanda, kwenye Maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani kwa mwaka 2024, yaliyofanyika katika mji mdogo wa Ushirombo, Wilayani Bukombe mkoani Geita Octoba 11, 2024. Kutoka kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Geita Martin Shigela, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA YAITEMBELEA TSC KUPATA UZOEFU WA UTENDAJI KAZI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa ufafanuzi wa namna TSC inavyotekeleza majukumu yake wakati wa ziara ya Naibu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama aliyoifanya katika ofisi za TSC tarehe 1 Oktoba, 2024.

Na mwandishi wetu – Dodoma.

Naibu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Bibi Alesia Mbuya ametembelea Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa lengo la kujifunza namna TSC inavyotekeleza majukumu yake katika kusimamia Walimu.

Naibu Katibu huyo aliyeambatana na afisa kutoka Tume hiyo, Bibi Salome Stephano ametembelea TSC tarehe 1 Oktoba, 2024 na kupokelewa na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama ambapo pamoja na mambo mengine Bibi Alesia alipata fursa ya kukutana na Kamati Maalum ya TSC inayohusika na kuchambua rufaa za walimu.

Bibi Alesia alisema kuwa lengo la kufanya ziara hiyo ni kujifunza namna ambavyo TSC inatekeleza majukumu yake ikiwa ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu kwa kuwa majukumu yake yanaendana na yale ya Tume ya Utumishi wa Mahakama ambayo ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Watumishi wa Mahakama.

Alieleza kuwa kuna maeneo

makuu matatu ambayo Tume ya Utumishi wa Mahakama inapenda kuyafahamu kwa kina ambayo ni Muundo wa Tume ya Utumishi wa Walimu, namna mashauri ya nidhamu yanavyoendeshwa na Sheria ya Tume ya Utumishi wa

Walimu Sura 448 kwa ujumla wake.

Kwa upande wa Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa pamoja na kwamba TSC na Tume ya Mahakama kila moja inatekeleza sheria yake, Taasisi hizo pia kuna wakati hulazimika kutumia Sheria ya Tume ya Utumishi wa Umma Sura 298 ambayo ndiyo Sheria mama katika kusimamia Utumishi wa Umma.

“Ni muhimu sana kwa Tume ya Utumishi wa Walimu na Tume ya Utumishi wa Mahakama kukutana na kupeana uzoefu kwa kuwa tunatekeleza majukumu yanayoendana. Kubadilishana uzoefu kunatoa fursa ya kila upande kujifunza kutoka kwa mwenzake kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa wetu,” alisema Mwl. Nkwama.

Katika Kikao hicho TSC iliwasilisha mada juu ya Muundo na Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Taratibu za Uendeshaji wa Vikao vya Tume na Kamati za Tume za Wilaya, Mchakato wa Nidhamu kwa Walimu pamoja na Mchakato wa Rufaa.



Naibu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Bibi Alesia Mbuya akizungumza jambo wakati wa kikao na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika tarehe 1 Oktoba, 2024 katika Ofisi za Katibu wa TSC jijini Dodoma.

TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA YAITEMBELEA TSC KUPATA UZOEFU WA UTENDAJI KAZI



Mkurugezi wa Kitengo cha Huduma za Sheria Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo akitoa ufafanuzi wakati wa kikao kilichowakutanisha baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya TSC na watendaji kutoka Tume ya Utumishi wa Mahakama tarehe 1 Oktoba, 2024 katika ofisi ya Katibu wa TSC jijini Dodoma.



Kikao kati ya baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na watumishi kutoka Tume ya Utumishi wa Mahakama kikiwa kinaendelea katika Ofisi ya Katibu wa TSC jijini Dodoma tarehe 1 Oktoba, 2024.



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Fatuma Muya akitoa wasilisho juu ya Taratibu za kuendesha Vikao vya TSC na Kamati zake wakati wa ziara ya Naibu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Bibi Alesia Mbuya (hayupo pichani) aliyoifanya TSC tarehe 1 Oktoba 2024.

TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA YAITEMBELEA TSC KUPATA UZOEFU WA UTENDAJI KAZI



Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Maadili na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Asha Lubuva (wa kwanza kushoto) akiwasilisha mada juu ya Muundo wa TSC wakati wa ziara ya Naibu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Bibi Alesia Mbuya aliyoifanya TSC tarehe 1 Oktoba 2024.



Afisa Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Selina Magoiga (kulia) akiwasilisha mada juu Mchakato wa Nidhamu kwa Walimu wakati wa ziara ya Naibu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Bibi Alesia Mbuya (hayupo pichani) aliyoifanya TSC tarehe 1 Oktoba 2024.



Afisa kutoka Tume ya Utumishi wa Mahakama, Bibi Salome Stephano akizungumza wakati wa kikao kazi kati ya Kamati ya kuchambua rufaa za walimu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na watendaji wa Tume ya Utumishi wa Mahakama kilichofanyika tarehe 1 Oktoba, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC jijini Dodoma.

WALIMU WAKUU WILAYANI MUHEZA WATAKIWA KUTAMBUA VIPAJI VYA WANAOWAONGOZA



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Bi. Zainabu Abdallah (kushoto) akiwasili katika Ukumbi wa Sunrise wilayani Muheza tarehe 25 Oktoba, 2024, kwa ajili kufungua mafunzo ya siku moja yaliyolenga kutoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 113 wa Shule za Msingi.

Na Mwandishi Wetu – Muheza.

Walimu Wakuu wilayani Muheza w a m e t a k i w a kutambua na kutumia vipaji vya walimu wanaowaongoza ili kuboresha mazingira ya kufundisha na utoaji wa elimu kwa wanafunzi wao.

Kauli hiyo imetolewa tarehe 25 Oktoba, 2024 na Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Bi. Zainabu Abdallah wakati akifungua mafunzo ya siku moja yaliyohusu ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 113 wa Shule za Msingi.

Alisema kuwa Mwalimu Mkuu wa Shule ambaye atatambua vipaji walivyonyesha walimu wake mbalimbali na kuviunganisha atakuwa na timu nzuri ambayo itasaidia shule yake kupata ushindi katika matokeo mbalimbali ya mitihani.

Bi. Zainabu aliongeza kuwa

kitendo cha baadhi ya Walimu Wakuu kuona Wivu kutokana na vipaji wanavyoonyesha walimu walio chini yao wakati wa kufundisha wanafunzi vinarudisha nyuma maendeleo ya elimu na kuwakatisha tamaa walimu wa namna hiyo.

“Mkuu wa Shule tambua talanta na vipaji vya kila mwalimu wako na vitumie kutengeneza timu ya ushindi...Mwalimu Mkuu hutakiwi kuona wivu pale unapoon Mwalimu wa chini yako anatumia kipaji chake kufanikisha ufundishaji bora kwa kuwa mafanikio ya kipaji chake yatakuletea sifa hata wewe,” alisisitiza.

Bi. Zainabu aliwataka Walimu Wakuu hao kwa nafasi zao kama viongozi hawana haja kuwaonea wivu waliochini yao na kutengeneza vipasuko bali wanatakiwa kuwaanda kuwa viongozi katika sekta mbalimbali kwa kuwawekea mipango inayowatayarisha kubeba majukumu ya uongozi.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Muheza aliwataka kuhakikisha Walimu Wakuu na Watumishi kuhakikisha wanalinda kazi yao kwa gharama yoyote kwa kuwa ndio chanzo ya heshima yao katika jamii.

Awali Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa jukumu la walimu Wakuu ni kuhakikisha wanawasimia walimu waliochini yao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa Walimu.

Alisema kuwa Walimu Wakuu kabla ya kuchukua hatua dhidi ya walimu wanaoonekana kuishi bila kufuata maadili na miiko ya walimu ni vyema wakawaelimisha kwanza na kujua chanzo cha changamoto ya mwalimu kukiuka maadili.

Mwl. Paulina alisema kuwa ni jukumu lao la kuhakikisha kuwa walimu wanatekeleza majukumu yao ya msingi ya kulea na kutoa ujuzi kwa kuzingatia maadili.

WALIMU WAKUU WILAYANI MUHEZA WATAKIWA KUTAMBUA VIPAJI VYA WANAOWAONGOZA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo ya awali tarehe 25 Oktoba, 2024, wakati wa mafunzo ya siku moja yaliyohusu ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 113 wa Shule za Msingi.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Bi. Zainabu Abdallah akifungua mafunzo ya siku moja tarehe 25 Oktoba, 2024 yaliyohusu ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 113 wa Shule za Msingi.



Baadhi ya Walimu Wakuu kutoka Shule za Msingi 113 za Wilaya ya Muheza, Mkoani Tanga wakifuatilia hotuba ya Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Bi. Zainabu Abdallah (hayupo katika picha) wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku moja yaliyolenga kutoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 113 wa Shule za Msingi.

NEEMA YAWASHUKIA WALIMU 690 WILAYA YA MISSENYI, WAPANDISHWA VYEO

Na Mwandishi wetu – MISSENYI.

Katika jitihada za Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kushughulikia maslahi ya walimu nchini amewapandisha vyeo walimu 690 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera katika kipindi cha 2023/24.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Missenyi, Bw. Gerald Kigundu wakati wa mahojiano na Maafisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo lkupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Alisema kuwa kati ya walimu waliopandishwa vyeo kwa mwaka 2023/24 wa shule za Msingi walikuwa 439 na Sekondari walikuwa 251.

Aliongeza kuwa katika mwaka 2023/24 jumla ya walimu 67 walisajiliwa ambapo wa Shule za Msingi walikuwa 34 na Sekondari 33, walimu 67 walithibishwa kazini na jumla ya walimu 24 waliobadilishiwa vyeo wakiwa wa shule za Msingi 23 na Sekondari mmoja (1).

Bw. Kigundu alieleza kuwa hatua alizochukua Rais Samia katika kulinda maslahi ya walimu, kwa upande wa Missenyi zimesaidia walimu kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

“Rais Samia ameweka historia ya pekee katika wilaya yetu kwa kuhakikisha haki na maslahi ya walimu yanalindwa kwa nguvu zote. Tukiangalia mwaka 2023/24 tulipandisha vyeo walimu 704 hii ni hatua kubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu,” alisema.

Alifafanua dhamana ya kupandisha vyeo walimu ipo mikononi mwa Kamati ya TSC Wilaya kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 huku akibainisha kuwa kwa upande wa Kyerwa kamati hiyo ilihakikisha kuwa kila mwalimu aliyekuwa na sifa ya kupanda cheo kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa alipata haki hiyo.

Pamoja na hayo, Katibu Msaidizi huyo alisema Rais Samia ameendelea kupunguza changamoto ya upungufu wa walimu katika Wilaya ya Misenyi kwa kuruhusu walimu kuajiriwa ambapo katika kipindi cha 2023/24 jumla ya walimu 67 wa ajira mpya walipangiwa vituo vya kazi katika wilaya hiyo.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, Bw. Gerald Kigundu alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kyerwa imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

“Tumefanikiwa kutembelea shule 53 ambapo 47 ni za msingi na 9 ni za sekondari. Katika ziara hizo tumekutana na walimu 282 wa shule za Msingi na



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Missenyi, Bw. Gerald Kigundu akiwa anatekeleza majukumu ya ofisi yake wilayani Missenyi hivi karibuni.

135 wa shule za Sekondari. Vilevile tumefanikiwa kusambaza kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu katika shule zote za msingi 103 Jitihada zote hizi ni kusaidia walimu kutekeleza majukumu yao bila kukiuka miiko ya kazi yao,” alisema.

Aliendelea kusema pamoja na jitihada hizo wapo baadhi ya walimu wachache ambao mienendo yao ilikuwa kinyume na maadili ya kazi ya ualimu jambo lililosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu.

Bw. Kigundu alifafanua kuwa jumla ya mashauri ya kinidhamu 19 yalipokelewa ambapo katika mwaka wa 2021/22 walipokea mashauri 06, 2022/23 shauri mmoja, mwaka 2023/24 hakukuwa na shauri na mwaka 2024/25 wameshapokea mashauri 12.

“Katika kipindi cha miaka minne, mashauri ya nidhamu 19 yalifunguliwa ambapo walimu 02 waliopatikana na hatia na kupewa adhabu ya kufukuzwa kazi. Mwalimu 01 alishushwa cheo,” alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Missenyi inahudumia jumla ya shule 127 zikiwemo 103 za msingi na 24 za Sekondari huku idadi ya walimu ikiwa ni 1,158 kwa shule za msingi ni 750 kwa upande wa sekondari ni 408.

NEEMA YAWASHUKIA WALIMU 690 WILAYA YA MISSENYI, WAPANDISHWA VYEO



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Missenyi, Bw. Gerald Kigundu (kulia) akiwa na Afisa Maadili, Bw. Dickson Martine (katikati) na Afisa Ajira Bi. Gaudensia Masota (kushoto) wakiwa katika majukumu yao kwenye Ofisi ya Tume ya utumishi wa Walimu Wilaya Missenyi.

WALIMU WAKUU WA SHULE ZA MSINGI WILAYANI TANGA WATAKIWA KUWA MFANO BORA KATIKA MAADILI



Mthibiti Mkuu wa Ubora wa Shule ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tanga, Bi. Mariam Masanja akifungua mafunzo ya siku moja tarehe 26 Oktoba, 2024 yaliyolenga kutoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu.

Na Mwandishi Wetu – Tanga.

Wakuu wa Shule za Msingi za Wilaya ya Tanga wametakiwa kuwa mfano wa kuigwa katika kuzingatia maadili yanayosimamia utumishi wa walimu na umma wakati wa utekelezaji wa majukumu katika maeneo ya kazi na jamii wanapoishi.

Kauli hiyo imetolewa tarehe 26 Oktoba, 2024 na Mthibiti Mkuu wa Ubora wa Shule ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tanga, Bi. Mariam Masanja wakati akifungua mafunzo ya siku

moja yaliyokuwa yakitoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu.

Alisema kuwa Wakuu wa Shule wanatakiwa kutambua kuwa wao ndio Mamlaka ya kwanza ya Nidhamu kwa walimu na hivyo ufanisi wa Tume ya Utumishi wa Walimu unategemea jitihada zao ikiwemo za wadau wengine katika kuhakikisha kuwa walimu wanazingatia miiko na maadili ya kazi zao.

Bi. Mariam aliwataka Wakuu hao wa Shule za Msingi kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu

zinazosimamia utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu.

Bi. Mariam aliwataka Walimu Wakuu kuhakikisha wanatumia mafunzo waliyopatiwa ili kuwaelimisha walimu wanaowaongoza kwa ajili ya kuwaepusha kujiingiza katika mashauri ya kinidhamu kwa sababu ya kutokuwa na elimu.

Awali, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tanga, Bi. Naima Abtwalib alisema kuwa jumla ya Wakuu wa shule za Msingi 81 wanashiriki mafunzo hayo yanayolenga kuwaongezea uwezo katika kusimamia maadili kwa walimu wanaowaongoza.

WALIMU WAKUU WA SHULE ZA MSINGI WILAYANI TANGA
WATAKIWA KUWA MFANO BORA KATIKA MAADILI

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tanga, Bi. Naima Abtwalib akitoa maelezo ya awali tarehe 26 Oktoba, 2024 kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi afunguea mafunzo yaliyolenga kutoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu.



Mthibiti Mkuu wa Ubora wa Shule ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tanga Bi. Mariam Masanja (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wakuu wa Shule wa Wilaya Tanga tarehe 26 Oktoba, 2024, mara baada ya kufungua mafunzo ya siku moja yaliyokuwa yakitoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 81 wa Shule za Msingi.



Baadhi ya Wakuu wa Shule za Msingi 81 za Wilaya ya Tanga wakifuatilia tarehe 26 Oktoba, 2024, mafunzo ya siku moja yaliyolenga kutoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu.

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AWAPA TABASAM WALIMU 920 WILAYA YA BIHARAMULO KWA KUWAPANDISHA VYEO



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Biharamulo, Bw. Fulko Hyera akiwa ofisini kwake.

Na Mwandishi wetu – Biharamulo.

Katika jitihada za Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kushughulikia maslahi ya walimu nchini amewapandisha vyeo walimu 920 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera katika mwaka wa fedha 2023/24.

Hayo yameelezwa na Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Biharamulo, Bw. Fulko Hyera wakati wa mahojiano na Maafisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Alisema kuwa kati ya walimu waliopandishwa vyeo kwa Shule za msingi ni 604 na Sekondari 316.

Bw. Hyera aliongeza kuwa katika mwaka 2023/24 jumla ya walimu 113 walisajiliwa ambapo wa Shule za Msingi walikuwa 85 na Sekondari 28, walimu 112 walithibishwa kazini na jumla ya walimu 60 waliobadilishiwa vyeo wakiwa wa shule za Msingi 49 na Sekondari 11.

Alieleza kuwa hatua alizochukua Rais Samia katika kulinda maslahi ya walimu, kwa upande wa Biharamulo zimesaidia walimu kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri

katika masomo yao.

“Rais Samia ameweka historia ya pekee katika wilaya yetu kwa kuhakikisha haki na maslahi ya walimu yanalindwa kwa nguvu zote. Tukiangalia mwaka 2023/24 tulipandisha vyeo walimu 920 hii ni hatua kubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu,” alisema.

Alifafanua dhamana ya kupandisha vyeo walimu ipo mikononi mwa Kamati ya TSC Wilaya kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 huku akibainisha kuwa kwa upande wa Biharamulo Kamati hiyo ilihakikisha kuwa kila mwalimu aliyekuwa na sifa ya kupanda cheo kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa alipata haki hiyo.

Pamoja na hayo, Katibu Msaidizi huyo alisema Rais Samia ameendelea kupunguza changamoto ya upungufu wa walimu katika Wilaya ya Biharamulo kwa kuruhusu walimu kuajiriwa ambapo kwa mwaka 2022/23 jumla ya walimu 113 wa ajira mpya walipangiwa vituo vya kazi.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, Bw. Hyera alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Biharamulo imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

“Tumefanikiwa kutembelea shule 15 ambapo 10 ni za msingi na 05 ni za sekondari. Katika ziara hizo tumekutana na walimu 175 wa shule za Msingi na 95 wa shule za Sekondari. Vilevile tumefanikiwa kusambaza kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu katika shule zote za msingi 117. Jitihada zote hizi ni kusaidia walimu kutekeleza majukumu yao bila kukiuka miiko ya kazi yao,” alisema.

Aliendelea kusema pamoja na jitihada hizo wapo baadhi ya walimu wachache ambao mienendo yao ilikuwa kinyume na maadili ya kazi ya ualimu jambo lililosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu.

Bw. Hyera alifafanua kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Julai 2024 TSC wilaya ya Biharamulo ilipokea na kushughulikia jumla ya mashauri 35 ambapo mashauri 27 yalithimishwa huku walimu 17 wakipewa adhabu ya kufukuzwa kazi, walimu 02 walipewa adhabu ya Kushushwa cheo, walimu 03 waliondolewa mashtaka, walimu 02 walirejeshwa kazini, mwalimu 01 alipewa adhabu ya kushushwa nyongeza ya mshahara na walimu wengine 02 waliondolewa mashtaka katika hatua ya uchunguzi wa awali.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Biharamulo inahudumia jumla ya shule 140 zikiwemo 117 za msingi na 23 za Sekondari huku idadi ya walimu ikiwa ni 1,743 huku walimu 1,261 wakiwa ni wa shule za msingi na walimu 482 ni wa shule za sekondari.

**RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AWAPA TABASAM WALIMU
920 WILAYA YA BIHARAMULO KWA KUWAPANDISHA VYEO**

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Biharamulo, Bw. Fulko Hyera akitoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo ofisini kwake hivi karibuni.

MUHEZA IMEPOKEA SHILINGI BILIONI 16 KWA AJILI YA MAENDELEO YA ELIMU



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Bi. Zainabu Abdallah wakati akifungua mafunzo ya siku moja yaliyokuwa yakitoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 113 wa Shule za Msingi.

Na Mwandishi Wetu – Muheza

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha miaka mitatu imetoa kiasi cha shilingi bilioni 16 kwa Wilaya ya Muheza kwa ajili ya maendeleo ya Elimu.

Kauli hiyo imetolewa tarehe 25 Oktoba, 2024 na Mkuu wa Wilaya ya Muheza Bi. Zainabu Abdallah wakati akifungua mafunzo ya siku moja yaliyohusu ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu.

Alisema kuwa kiasi cha shilingi bilioni 5 zilikuwa ni kwa ajili ya kulipia ada kwa wanafunzi kuanzia shule za Msingi hadi kidato cha sita.

Bi. Zainabu alisema kuwa hatua hiyo imesaidia kuondoa changamoto iliyokuwa ikiwakumba wananchi ya kutafuta ada kila ilipofika mwezi Desemba ya kila mwaka.

“Tunamshukuru sana Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake kubwa za kuhakikisha kuwa sekta ya elimu inapaa na wanafunzi na walimu wanakuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufundishia kwa kupeleka fedha nyingi katika maeneo mbalimbali ili kuboresha maendeleo ya elimu,” alisema.

Alisema kuwa kufuatia jitihada hizo, Serikali ya Muheza inaendelea na kampeni ya kuhamasisha maendeleo inayojulikana kama

“Mtoto wa leo Samia wa Kesho ambayo inalenga kuchochea maendeleo ya elimu kwa kuboresha ufaulu kwa wanafunzi.

Katika hatua nyingine Bi. Zainabu aliwashukuru Wakazi wa Wilaya ya Muheza kwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa ya kuifanya kufikisha asilimia 126 na hivyo kuwa ya pili nchini baada ya Wilaya ya Dodoma ambayo imefikia asilimia 128.

Aliwataka kutumia fursa kujitokeza tarehe 27 Novemba, 2024 kwa ajili ya kupiga kura za kuwachagua viongozi mbalimbali wa vijiji, mitaa na vitongoji ili ikiwezekana ichukuea namba moja kitaifa.

MUHEZA IMEPOKEA SHILINGI BILIONI 16 KWA AJILI YA MAENDELEO YA ELIMU



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Bi. Zainabu Abdallah (katikati) akiwa katika picha ya pamoja tarehe 25 Oktoba, 2024 na Walimu Wakuu kutoka Shule za Msingi za Wilaya hiyo baada ya kufungua mafunzo ya siku moja yaliyolenga kutoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 113 wa Shule za Msingi.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Bi. Zainabu Abdallah (kushoto) akiagana na viongozi mbalimbali wa Tume ya Utumishi wa Walimu mara baada ya kumaliza ufunguzi wa mafunzo ya siku moja yaliyolenga kutoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 113 wa Shule za Msingi.

WALIMU 1,556 WAPANDISHWA VYEO BUKOBA

Na Mwandishi wetu – Bukoba.

Katika jitihada za Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kushughulikia maslahi ya walimu nchini amewapandisha vyeo walimu 1,556 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera katika mwaka wa fedha cha 2023/24.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bukoba, Bw. Edwin C. Karumuna wakati wa mahojiano na Maafisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Alisema kuwa kati ya walimu waliopandishwa vyeo kwa mwaka 2023/24 wa shule za Msingi walikuwa ni 888 na Shule za Sekondari ni 668.

Bw. Karumuna alisema kuwa jumla ya Walimu 90 wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba walithibitishwa kazini ambapo Walimu wa Shule za Msingi ni 32 na Walimu wa Shule za Sekondari ni 58.

Alisema kuwa katika kipindi hicho, jumla ya Walimu 71 walibadilishwa vyeo katika Wilaya ya Bukoba, kati ya hao Shule za Msingi ni 67 na Shule za Sekondari ni 4.

Bw. Karumuna aliongeza kuwa hatua alizochukua na Rais Samia katika kulinda maslahi ya walimu, kwa upande wa Bukoba zimesaidia walimu kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

“Rais Samia ameweka historia ya pekee katika wilaya yetu kwa



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bukoba, Bw. Edwin C. Karumuna akitoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo ofisini kwake hivi karibuni.

kuhakikisha haki na maslahi ya walimu yanalindwa kwa nguvu zote. Tukiangalia mwaka 2023/24 tulipandisha vyeo walimu 1,556 hii ni hatua kubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu,” alisema.

Alifafanua dhamana ya kupandisha vyeo walimu ipo mikononi mwa Kamati ya TSC Wilaya kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 huku akibainisha kuwa kwa upande wa Wilaya ya Bukoba kamati hiyo ilihakikisha kuwa kila mwalimu aliyekuwa na sifa ya kupanda cheo kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa alipata haki hiyo.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, Bw. Karumuna alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Bukoba imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi

wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

Alisema kuwa pamoja na jitihada hizo wapo baadhi ya walimu wachache ambao mienendo yao ilikuwa kinyume na maadili ya kazi ya ualimu jambo lililosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu.

Bw. Karumuna alifafanua kuwa katika mwaka wa 2021/22 hadi mwaka 2023/24 walimu 27 walifukuzwa kazi, walimu wawili (02) walishushwa vyeo na mwalimu mmoja alipewa adhabu ya kukatwa asilimia 15 ya mshahara kwa kipindi cha miaka mitatu.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Bukoba inahudumia jumla ya walimu 2720 ambao Walimu wa shule za Msingi ni 1598 na Walimu wa Shule za Sekondari ni 1122.

WALIMU 1,556 WAPANDISHWA VYEO BUKOBA



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bukoba, Bw. Edwin C. Karumuna akitoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo ofisini kwake hivi karibuni.

SERIKALI IMEPANDISHA VYEO ZAIDI YA NUSU YA WALIMU NCHINI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo ya awali tarehe 26 Oktoba, 2024 wakati wa mafunzo ya siku moja yaliyokuwa yakitoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 81 wa Shule za Msingi.

Na Mwandishi Wetu – Tanga.

Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweza kuwapandisha vyeo Walimu 158,916 wa shule za Umma za Sekondari na Msingi.

Kauli hiyo imetolewa tarehe 25 Oktoba, 2024 na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama wakati wa mafunzo ya siku moja yaliyolenga kutoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 81 wa Shule za Msingi.

Alisema kuwa idadi hiyo ni zaidi ya nusu ya walimu wa shule za umma za Msingi na Sekondari 274,000 wanaohudumiwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) nchini.

Mwl. Paulina alimshukuru Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa tangu aiingie madarakani kwa kipindi cha maika mitatu amefanyakazi nzuri ya kutatua changamoto za walimu zikiwemo suala la madaraja ambapo kwa sasa changamoto hiyo imekuwa ni historia.

Aliongeza kuwa katika kuboresha elimu nchini, Rais Samia pia aliwezesha upatikanaji wa Dola za kimarekani bilioni 1.15 chini ya Mradi wa 'Boost', fedha zilizosaidia kuwajengea uwezo walimu wakuu wa Shule za Msingi nchini.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa mafunzo hayo ni muhimu sana kwa walimu Wakuu kwa ajili ya kupata elimu ambayo itawawezesha walimu wanaowaongoza ili waweze kufanya kazi zao kwa kuzingatia miiko na maadili yanayosimamia utendaji wa walimu na utumishi wa umma.

Alisema kuwa hatua hiyo

itasaidia kuwaepusha walimu kujiingiza katika mashauri kwa sababu ya ukosefu wa elimu juu ya kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu.

"Kwa kweli sisi TSC tunasikitika kuona kuwa baadhi ya walimu wanapungua kwa sababu ya kuvunja miiko na kukiuka maadili katika utumishi wa walimu... hivyo mafunzo yawe chachu ya kuzuia tatizo hilo kujitokeza labda kwa yule ambaye kwa makusudi atakuwa amepata elimu na anaamua kukiuka," alisema.

Katika hatua nyingine Mwl. Paulina Nkwama aliwataka Walimu kutokopa kupita kiasi kilichokubaliwa kwa mujibu wa taratibu za utumishi wa umma.

Alisema kuwa kukopa kupita kiasi kumesababisha ukosefu wa utulivu kwa baadhi ya walimu na kuwasababisha kushindwa kuwajibika ipasavyo katika maeneo yao ya kazi.

SERIKALI IMEPANDISHA VYEO ZAIDI YA NUSU YA WALIMU NCHINI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika picha ya pamoja na Wakuu wa Shule wa Wilaya Tanga tarehe Oktoba, 2024, baada ya kutoa maelezo katika mafunzo ya siku moja yaliyokurwa yakitoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwa Walimu Wakuu 81 wa Shule za Msingi.



Baadhi ya Wakuu wa Shule za Msingi 81 za Wilaya ya Tanga wakifuatilia tarehe 26 Oktoba, 2024 mafunzo ya siku moja yaliyolenga kutoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu